UCHUMI WA BULUU

MWANANCHI

# Bandari ya uvuvi kuanza kujengwa mwezi ujao

Mwandishi Wetu, Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

**Lindi.** Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki amewataka wananchi wilayani Kilwa kujipanga kuzitumia vyema fursa zitakazojitokeza wakati wa ujenzi wa bandari ya uvuvi unaotarajiwa kuanza mwezi ujao.

Waziri Ndaki alisema hayo alipokagua eneo lililotengwa kwa ajili ya ujenzi wa bandari hiyo. Akiongea na wananchi, alisema kuanza kwa ujenzi wa mradi huo kutaam-batana na fursa zenye manufaa kwao hivyo wajiandae ili kuwa sehemu ya wanufaika badala ya watazamaji.

"Naomba muiamini Serikali yetu makini, Rais Samia Suluhu Hassan amedhamiria kujenga Tanzania. Huu ni mradi wake wa kielelezo, wakimkakati na utakaoacha ala-ma kwenye nchi hii," alisema Ndaki.

Serikali imetenga zaidi ya Sh100 bilioni kujenga bandari hiyo na waziri aliwataka wananchi wa Kilwa kujiandaa kuchangamkia fursa zitakazojitokeza wakati wa ujanzi.

Waziri Ndaki aliwataka wananchi wanaotakiwa kuachia maeneo kutokuwa na wasiwasi kwani Serikali itahakikisha kila mmoja anapata haki yake.

Awali, akitoa taarifa namna walivyojiandaa, Mkuu wa Wilaya ya Kilwa, Zainab Kawawa alisema matayarisho yote yamekamilika na wananchi wanaotakiwa kuupisha mradi huo wapo tayari kuondoka.

"Tunaamini bandari hii itakapojengwa na kukamilika italeta tija kubwa kwa wavuvi na wananchi kwa ujumla, na sisi tumeshafanya matayarisho yote ili mradi huu usikwame," alisema Zainabu.

Mmoja wa wavuvi waliokuwapo eneo hilo la mradi, Suleiman Mohammed alisema uvuvi wanaoufanya Bahari ya Hindi hauna uhaki-ka wa kuuza samaki wanaowapata kwani soko lililojengwa kwa ajili ya shughuli hiyo mpaka leo halijaanza kutumika.

"Tunaomba soko hili lianze kufanya kazi tu-fanyie biashara hapo," alisema Mohammed.

**FURSA KEMKEM ZA UCHUMI**

**Tanzania inao ufukwe wenye urefu wa zaidi ya kilomita 1,400 unaoanzia mkoani Tanga mpaka Mtwara hivyo kutoa fursa kwa wananchi wa mwambao kuvua na kufanya shughuli nyingine za kiuchumi. Hata hivyo, kwa muda mrefu wengi wamekuwa wakifanya uvuvi mdogo jambo lililoishawishi Serikali kuwekeza kwenye miundombinu itakayowavutia wafanyabiashara kushiriki uvuvi wa bahari kina wenye fursa kubwa zaidi ya zinazopatikana sasa kwa wavuvi wadogo wanaovua kwa zana duni.**

CamScanner

# Bilioni 100/- kujenga bandari Uvuvi Kilwa

NIPASHE

**Na Mbaraka Kambona,**
KILWA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki amewataka wananchi hususan wanaoishi wilayani Kilwa kujipanga kutumia vyema fursa zitakazojitokeza wakati wa utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Bandari ya Uvuvi utakaoanza mwezi Juni, mwaka huu.

Waziri Ndaki alitoa wito huo alipofanya ziara ya kutembelea na kukagua eneo lililotengwa kwa ajili ya ujenzi wa bandari hiyo lililopo wilayani Kilwa, mkoani Lindi, mwishoni mwa wiki.

Wakati akiongea na wananchi wa wilaya hiyo, alisema kuanza kwa ujenzi wa mradi huo kutaambatana na fursa mbalimbali zitakazo kuwa na manufaa kwao na kwamba ni vyema wananchi hao wakaanza kujiandaa ili mradi utakapoanza waweze kuwa sehemu ya wanufaika na sio watazamaji.

Alisema katika kuhakikisha mradi huo unajengwa na kukamilika, Rais Samia Suluhu Hassan ameridhia kutengwa kiasi cha pesa kisichopungua bilioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa bandari hiyo. "Naomba muiamini serikali ya Mama yetu makini, Rais Samia Suluhu Hassan, amedhamiria kujenga Tanzania, huu ni mradi wake wa kielelezo, wa kimkakati na utakaoacha alama kwenye nchi hii," alisema.

Waziri Ndaki aliwahakikishia wananchi wa Kilwa kuwa bandari hiyo itaanza kujengwa mapema mwezi Juni mwaka huu na aliwataka kujiandaa kuchangamkia fursa mbalimbali zitakazojitokeza wakati mradi huo unatekelezwa.

Awali, akitoa taarifa ya wilaya ilivyojiandaa kuhakikisha mradi huo unajengwa, Mkuu wa Wilaya ya Kilwa, Zainab Kawawa, alisema wameshafanya matayarisho yote kuhakikisha mradi huo unajengwa na wanaotakiwa kuachia maeneo yao kupisha mradi huo wapo tayari kufanya hivyo.

"Tunaamini kwamba bandari hii ya kimkakati itakapojengwa na kukamilika italeta tija kubwa kwa wavuvi na wananchi kwa ujumla na sisi tumeshafanya matayarisho yote ili mradi huu usikwame," alisema.

Naye, mvuvi anayefanya shughuli zake wilayani Kilwa, Suleiman Mohammed, akizungumza kwa niaba ya wenzake alisema ni kweli wanavuna samaki katika Bahari ya Hindi, lakini hawana sehemu ya uhakika ya kuuzia samaki wao kwa kuwa soko lililojengwa kwa ajili ya shughuli hiyo mpaka sasa halijaanza kutumika.

"Tunakuomba Mheshimiwa waziri soko hili lililojengwa lifanye kazi ili tuweze kulitumia kufanya biashara zetu," alisema Mohammed. Waziri Ndaki aliwataka wananchi wanaotakiwa kuachia maeneo yao kwa ajili ya kupisha mradi huo wasiwe na wasiwasi, serikali itahakikisha kila mmoja anapata haki yake anayostahili.

CamScanner

THE GUARDIAN



Livestock and Fisheries ministry (Fisheries) permanent secretary Dr Rashid Tamatamah (R, gesturing) shows Livestock and Fisheries minister Mashimba Ndaki (L) in Kilwa District, Lindi Region, at the weekend an area set aside for the construction of a fisheries port. The minister said the government has allocated 100bn/- to the project, whose implementation will begin early next month. Photo: Correspondent Mbaraka Kambona

CamScanner

# Wananchi watakiwa kujiandaa ujenzi Bandari ya Uvuvi Kilwa

**Na MWANDISHI WETU**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amewataka wananchi hususan wanaoishi wilayani Kilwa kujipanga kutumia vema fursa zitakazojitokeza wakati wa utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Bandari ya Uvuvi, utakaoanza mwezi ujao.

Ndaki alisema hayo mwishoni mwa wiki alipofanya ziara ya alipokagua eneo lililotengwa kwa ujenzi wa bandari hiyo iliyopo wilayani Kilwa, mkoani Lindi.

Waziri huyo alisema kuanza kwa ujenzi wa mradi huo kutaambatana na fursa zitakazokuwa na manufaa kwao, hivyo ni vema wananchi wakaanza kujiandaa ili mradi utakapoanza wawe sehemu ya wanufaika na siyo watazamaji.

Aliongeza katika kuhakikisha mradi huo unajengwa na kukamilika, Rais Samia Suluhu Hassan ameridhia kutengwa sh. bilioni 100 za ujenzi wa bandari hiyo.

> **Naomba muiamini serikali ya mama yetu makini, Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kuwa imedhamiria kujenga Tanzania, huu ni mradi wake wa kielelezo, wa kimkakati utakaoacha alama katika nchi hii...**
>
> Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki

UHURU

"Naomba muiamini serikali ya mama yetu makini, Rais Samia Suluhu Hassan, kuwa kuwa imedhamiria kujenga Tanzania, huu ni mradi wake wa kielelezo, wa kimkakati utakaoacha alama katika nchi hii," alisema.

Waziri Ndaki aliwahakikishia wananchi wa Kilwa kuwa bandari hiyo itaanza kujengwa Juni, mwaka huu, hivyo wajiandae kuchangamkia fursa zitakazojitokeza wakati unatekelezwa.

Aidha, aliwatoa hofu wanaotakiwa kuachia maeneo yao kupisha mradi huo wasiwe na wasiwasi, kwa kuwa serikali itahakikisha kila mmoja anapata haki yake anayostahili.

Awali, akitoa taarifa ya namna wilaya ilivyojiandaa kuhakikisha mradi huo unajengwa, Mkuu wa Wilaya ya Kilwa, Zainab Kawawa, alisema wameshafanya matayarisho yote kuhakikisha unajengwa na wanaotakiwa kuachia maeneo yao kupisha mradi huo wapo tayari kufanya hivyo.

"Tunaamini kwamba bandari hii ya kimkakati itakapojengwa na kukamilika italeta tija kubwa kwa wavuvi na wananchi kwa ujumla, sisi tumeshafanya matayarisho yote ili mradi huu usikwame," alisema.

Suleiman Mohammed anayefanya shughuli za uvuvi wilayani Kilwa, akizungumza kwa niaba ya wenzake, alikiri kwamba wanavuna samaki Bahari ya Hindi, lakini hawana sehemu ya uhakika ya kuwauzia kwa kuwa soko lililojengwa kwa shughuli hiyo halijaanza kutumika.

"Tunakuomba Waziri soko hili lililojengwa lifanye kazi ili tulitumia kufanya biashara zetu," aliomba Mohammed.

